**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

**Simu - Utawala Na: +255 – 0768890896**
**Simu - Mafunzo Na: + 255 – 0787676981**
**Tovuti: www.fiti.ac.tz**
**Baruapepe: info@fiti.ac.tz**

**Chuo cha Viwanda vya Misitu,**
**S. L. P. 1925,**
**MOSHI.**

# FOMU YA MAOMBI YA HOSTELI 2025/2026

1. Taarifa za mwanafunzi:
   a) Jina kamili la Mwanafunzi..........................................................................
   b) Tarehe ya kuzaliwa....................................................................................
   c) Jinsia: Mwanaume/Mwanamke (kata isiyohusika)
   d) Kozi: Basic Technician Certificate/Technician Certificate/Ordinary Diploma (kata isiyohusika)
   e) Namba ya simu..........................................................................................
2. Taarifa za mzazi/mlezi:
   a) Jina kamili la Mzazi/Mlezi..........................................................................
   b) Sehemu anapoishi:
      Mkoa.............................. Wilaya...........................................
      Kijiji/Mtaa.....................................................................................
   c) Anuani kamili ya Mzazi/Mlezi......................................................................
   d) Namba ya simu ..........................................................................................
3. Orodhesha majina matatu ya ndugu zako wa karibu ambao kama kukiwa na dharura watajulishwa:

| Na. | Jina | Uhusiano | Namba ya simu |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |

## MASHARTI YA KUISHI HOSTELI

1. Wanafunzi wote watajiandikisha katika kitabu maalum kwa Msajili wa Wanafunzi siku wanaporipoti na kuonyesha stakabadhi ya malipo ya hosteli.
2. Usafi wa ndani ya chumba utafanywa na wanafunzi wanaoishi ndani ya chumba hicho.
3. Ni marufuku kupika kitu chochote ndani ya hosteli (kwa hiyo vitu vifuatavyo; birika za umeme, sufuria za umeme, na vifaa vingine vya aina hiyo haviruhusiwi ndani ya hosteli). Mwanafunzi atakayepatikana na vifaa hivyo atafukuzwa ndani ya hosteli na vifaa hivyo kuchukuliwa. Faini itatozwa kwa atakayekutwa na vifaa hivyo.
4. Ni marufuku kupiga kelele, kufungulia redio kwa sauti ya juu, kutumia lugha chafu, kupigana na vitendo vingine kama hivyo katika hosteli. Mwanafunzi atakayepatikana na makosa yaliyotajwa atakuwa amepoteza sifa za kuishi hosteli na malipo hayatarudishwa.
5. Wageni wote **hawaruhusiwi** kuingia ndani ya hosteli. Yeyote atakayevunja sheria hii atakuwa amepoteza sifa za kuishi hosteli hivyo atafukuzwa hoteli mara moja.
6. Mwanafunzi atakayemruhusu mwanafunzi mwenzake ambaye hana usajili wa chumba husika kulala kwenye chumba hicho atakuwa amepoteza sifa za kuishi ndani ya hosteli za chuo.
7. Kumbuka:
   a) Wizi, uasherati, ulevi, kupigana, matusi, utumiaji wa madawa ya kulevya au sigara, **hairuhusiwi na ikabainika utafukuzwa chuo.**
   b) Hairuhusiwi Mwanafunzi kuishi na mke, mume au na mtoto ndani ya hosteli za chuo.
   c) Utawala utafanya ukaguzi wa usafi na vitu vyote visivyoruhusiwa wakati wowote ndani ya hosteli.
8. Mkataba wa kuishi hostel ni wa mihula miwili hivyo mwanafunzi kwa sababu zake binafsi akiamua kuhama hosteli atatakiwa kukijulisha Chuo kwa barua na kulipa gharama za mwaka mzima shilingi laki tatu **(300,000)**

**Mwanafunzi atakayekiuka masharti ataadhibiwa kulingana na sheria za mwanafunzi za Chuo.**

**Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi baada ya kusoma na kukubaliana na masharti ya kuishi hosteli.**

Mimi................................................ (Jina la Mwanafunzi) naahidi kuwa nitafuata masharti na sheria za kukaa hosteli.

Sahihi. ................................ Tarehe..................................

**GHARAMA YA HOSTELI**

Gharama ya kuishi Hosteli kwa mwaka ni **Tshs 300,000/=.** Fedha hizi zitalipwa mara mbili (2), mwanzoni mwa muhula wa kwanza na mwanzoni mwa muhula wa pili. Mwanafunzi anapopata taarifa ya kukubaliwa kuishi hoteli atatakiwa kulipia gharama ya hosteli kwa kutumia **control number** atakayopewa. Kwa mahitaji ya Contorl number kwa ajili ya hostel wasiliana kwa namba hii **0768890896, 0717085141 OR 0695422570.**

Jaza fomu hii na kuituma kwa barua pepe: admission@fiti.ac.tz au fika ofisi ya Msajili wa Wanafunzi.

**KARIBU CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU**

..........................................

MKUU WA CHUO
CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU
MOSHI

**Dr. Zacharia J Lupala**
**MKUU WA CHUO**